

Pambazuko

Toleo Namba 073

Jumatatu Mei 20-26, 2024



Jicho la Tai

Achefukwa Makalla UK. 5 kupigia debe Chadema



**Bunge
Marekani
lagoma
kumwalika
Ruto** Uk. 10



**Rais
Tshisekedi
chupuchupu
kupinduliwa**
Uk. 18



Muongano fupa gumu

- Watishia usalama wa Tanzania
- Ni jaribio zito kwa Rais Samia

UK.13-17

TFF lawamani msiba wa Jellah Mtagwa

 Uk. 19

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Kutolipa madeni ya vyombo vya habari ni wizi

MTEJA mkubwa wa nafasi za matangazo kwenye vyombo vya habari; magazeti, redio na televisheni, ni serikali.

Kutokana na kuaminika kwake, mteja huyo – serikali, kupitia taasisi zake, amekuwa akifanya biashara na vyombo vya habari, bila kuwepo wasiwasi kwamba hatalipa.

Lakini kumbe imani hiyo haikupaswa kuwekwa kwa mteja huyo, kwani ameonyesha dharau ya kutolipa madeni baada ya kufanya biashara na vyombo hivyo.

Pambazuko tunasema ni dharau ya serikali kwa kuchelea kulipa madeni yake, kwa kuwa tunaamini uwezo wa kulipa, anao, bali amekomaza shingo yake kwa dharau na kiburi.

Haiwezekani kabisa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia taasisi zake, ikashindwa kulipa Shilingi bilioni 18 tu, tena madeni haya yakiwa ni ya muda mrefu sana.

Kukaidi kulipa madeni yake kwa vyombo vya habari kwa wakati, baada ya kupewa huduma, kunajenga taswira kwamba hata watu binafsi wanaweza wasilipe wanapopata huduma, hata kama wana uwezo wa kufanya hivyo.

Mara zote, serikali ndiye muongoza njia, lakini katika hili imekosa heshima na haipaswi kuigwa na yeyote kwa kuwa imekuwa mfano mbaya.

Mara kadhaa, viongozi wakuu wa serikali, akiwamo Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, wamekuwa wakihimiza kulipwa kwa madeni hayo, lakini hakuna kinachonekana kutekelezwa. Ni kiburi.

Yaani inaonekana kuwa hata taasisi za serikali nazo haziheshimu amri za wakubwa wao; rais na waziri mkuu, na zimekuwa ‘zikipuyanga’ tu bila wasiwasi wala kushtuka kutekeleza kauli za wakubwa hao kwamba walipe madeni yao.

Kana kwamba hiyo haitoshi, wiki iliyopita, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye naye wakati wa hotuba ya bajeti, alihimiza yaleyale ya wakubwa wake kwamba serikali ilipe madeni yake kwa vyombo vya habari.

Nape alisema taasisi ambazo zimepata huduma kutoka vyombo vya habari na kuacha kuvilipa, vinafanya uharamia ambao wizara yake haikubaliani nao.

Itambulike kuwa vyombo vingi vya habari, kwa kiasi kikubwa vinaendeshwa kwa kufanya biashara ya kuuza nafasi kwenye magazeti au muda kwenye vyombo vya kielektroniki, yaani redio na televisheni.

Ni kutokana na mapato ya matangazo hayo, vyombo hivyo vya habari vinaweza kulipa mishahara waandishi wake wa habari, wapigapicha na wafanyakazi wengine, kulipia umeme, maji na huduma zingine zinazopaswa kuwepo wakati wa uzalishaji wa vyombo hivyo.

Kutokana na kiburi hicho cha serikali kwa kutolipa madeni, sisi Pambazuko tunakubaliana na mapendekezo ya wabunge wengi kwamba kitengwe kiasi maalum cha fedha katika bajeti ambacho kitatumika kwa ajili ya kulipa madeni ya vyombo vya habari ili visife.

FURAHA NA MAMA ZANGU...



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wa Tanzania, January Makamba akifurahia jambo na Graca Machel, mjane wa aliyekuwa Rais wa Msumbiji, Samora Machel (kushoto), pamoja na Rais (mstaafu) wa Ireland, Mary Robinson. Viongozi hawa walikutana wiki iliyopita katika Jiji la Paris, Ufaransa. (Picha kutoka mtandao wa X).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Tupinge mfumo wa elimu unaomezesa propaganda. Tuhoji wimbo tunaousikia kila siku kutoka kwa baadhi ya wanasiasa kwamba elimu ijenge usalendo. Siyo kazi ya elimu kujenga usalendo. Kazi ya elimu ni kuzaa vijana wenye kipaji na ustadi wa kudadisi dhana zote pamoja na dhana ya usalendo na utafa. Kazi ya elimu ni kufikirisha, siyo kukumzesha fikra – Prof. Issa Shivji.

Tangazo**Tuchangie**

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

**Mhariri Mkuu,
Oktoba, 2023**

Changia Pambazuko liendelee

WAJUMBE: wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakituma fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokuwa zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukaza Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeviza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yamevekwa wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majeraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kumarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kusuzwa, lakini hasi kubaliana na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufika umma bure.

Sasa basi, endapo utapata changamoto kuendelea na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sava ya "asante" kutoka kwetu.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263

Ukitema mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandika: **Pambazuko Gazeti.** Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliowaomba kuchagia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263.**

Lipa kwa Simu

Lipa kwa kuscana

Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI

Logos: Airtel, Tigo, Safaricom, M-Pesa, Airtel Money, Airtel Salama

Achefukwa Makalla kupigia debe Chadema

“HIVI hawa watendaji wa chama changu wanajielewa kweli, wao wamekalia kushabikia vyama vya wapinzani, kila siku wakipewa kujipigia debe, wao wanapaisha vyama pinzani, hawajielewi hawa...

... Mimi wanani kwaza sana nimesema na kusema, lakini wao wanajifanya hawasikii. Kila mara nawafunza, lakini wao ni watu wasiojielewa...

... Tena hawa vijana ndiyo hovyoka kabisa, hawajawahi hata kupita Kivukoni chuoni, hawajui namna ya kutangaza chama chetu kila wanapopata nafasi.”

Haya ni maneno aliyoa nayo Mzee Tai jana wakati akitoka chumbani kwake. Hakutaka hata kuwajulia hali wasaidizi wake; kijana anayesaidia usafi na mapishi na hata mwandishi wake, ambao wote huishi nyumba moja.

Mzee Tai baada ya kutulia kidogo, akarejea sebuleni na kuomba aandaliwe chai ili astafutahi kabla hajaanza mazoezi yake; kutembea kuzunguka nyumba yake.

Akiwa ameketi kwenye kochi analopenda zaidi, akakaribishwa mezani kwa ajili ya kunywa chai. Wakati ananyanyuka, akaendelea kufoka.

“Haiwezekani mambo haya yakapita hivihivi, lazima suala hili lizungumzwe na kupigiwa kelele zaidi hadi mwenyekiti wa chama chetu cha mapinduzi asikie na ikiwezekana achukue hatua mapema...

...Mimi siwezi kukubali kuona mambo yakiparaganyika ndani ya CCM na nikakaa kimya, lazima niseme na nitasema sana na sitakaa kunyamaa. Nitasema tu, tena kwa sauti ya juu.

Mzee Tai badala ya kwenda mezani kwa ajilia ya kunywa chai, yeye akaongoza hadi chumbani kwake na kufunga mlango... akaubamzia mlango; phaaaa!

Baada ya muda kupita, kijana wake akamfuata chumbani na kumkaribisha upya kwa ajili ya chai. Kumbe alikuwa amesahau kuwa alikaribishwa kwa ajili



Amos Makalla

ya kustafutahi.

Akareja akiwa amevaa tisheti yake maarufu yenye picha ya Rais Samia Suluhu Hassan, ikiwa imebeba maneno haya; “Mitano Tena kwa Mama.”

Baada ya kuketi akamuita mwandishi wake na kumwamuru achukue kompyuta mpakato kwa ajili ya kuandika atakachoelekezwa.

“Hakikisha haya nayokueleza unayafikisha Pambazuko na yawafikie Watazania wote na watu wengine kote waliko kwa CCM wa Halmshauri Kuu – Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla.

Povu lote la Mzee Tai kumbe ilikuwa ni hasira baada ya kudai kukasirishwa na maneno aliyoitia ya kukipigia debe Chadema yaliyotoka kinywani mwa Katibu wa CCM wa Halmshauri Kuu – Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla.

Kwamba wakati Makalla akipewa kipindi ndani ya televisheni moja ya Dar es Salaam, kuelezea na kukitangaza chama chake cha CCM, yeye alitumia dakika nyingi zaidi kuitaja Chadema.

Mzee Tai eti alikasirika zaidi baada ya kudai kwamba Makalla alikitaja chama hicho cha upinzani mara 29, huku akikitaja chama chake mara 8 tu.

Habari

Wizara nyeti yaambulia asilimia 0.1 ya bajeti

Na Mwandishi WETU,
Dodoma

WIZARA inayoshughulikia mambo nyeti yanayohusu maadili ya taifa, imepangiwa kiasi kidogo cha fedha katika bajeti ya mwaka 2024/25.

Pambazuko linaeleza kuwa bajeti hiyo kiduchu, imesikitisha na kuhuzunisha wabunge wengi ambao wameilaumu serikali na kuituhumu kuwa haipo makini kuhusu masuala ya mmomonyoko wa maadili.

Kwamba mmomonyoko huo umekuwa chanzo cha madhila mengi ya kimaadili katika jamii ya Watanzania.

Wakijadili Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum bungeni jijini Dodoma wiki iliyopita, wabunge waliishangaa serikali kutenga asilimia 0.14 tu ya bajeti nzima ya serikali kwa ajili ya wizara hiyo ambayo ndio mhimili wa kulinda maadili ya jamii.

Katika bajeti hiyo, waziri wa wizara hiyo nyeti, Dkt. Dorothy Gwajima, aliomba Bunge kuidhinisha shilingi bilioni 67.905 kwa ajili ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Kiasi hicho ni asilimia 0.14 tu ya bajeti nzima ya serikali ambayo inatarajiwa kuwa takribani shilingi trilioni 49.5 kwa mujibu wa makadirio ya ukomo wa bajeti yaliyotangazwa na serikali mapema mwaka huu.

Kati ya fedha hizo zilizoombwa na wizara, shilingi bilioni 20.418 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambazo zitahusisha shilingi bilioni 18.025 kutoka ndani ya nchi na shilingi bilioni 2.392 za wafadhili na mikopo kutoka nje.

Wizara hiyo imepanga kutumia shilingi bilioni 47.487 kwa ajili ya matumizi ya kawaida zikijumuisha shilingi bilioni 25.836 za matumizi mengineyo na shilingi bilioni 21.65 za mishahara ya watumishi.



Prof. Mkenda

Katika michango yao wabunge walisema haishangazi kuona kuwa vitendo vya ubakaji, ulawiti, ushoga na mmomonyoko wa maadili kwa ujumla vikishamiri nchini kwa sababu wizara inayotakiwa kushughulikia mambo hayo haipatiwi bajeti ya kutosha na serikali.

Wabunge hao waliionyesha “kujawa” uchungu ambapo wamesema masuala ya ubakaji, ulawiti na ushoga hayaonekani kupitia hotuba ya bajeti ya wizara hiyo kiasi cha mbunge mmoja kumtaka Waziri Gwajima kuonyesha uchungu huo.

Katika hali ya utani, waziri huyo aliigiza kulia wakati akijibu hoja za wabunge.

Wabunge hao waliilaumu wizara hiyo na serikali kwa jumla kwa kuchukulia masuala ya mmomonyoko wa maadili katika jamii kama ‘jambo jepesi.’

Wakashauri kuwa ili kukomesha vitendo vinavyoharibu maadili ya jamii kama ubakaji, ushoga na ulawiti, basi sheria zibadilishwe ili kuweka adhabu kali kwa watu watakaopatikana na hatia ya makossa hayo.

“Sheria ibadilike ili wanaojihusisha na ubakaji na ulawiti wahasiwe,” alisisitiza Mbunge Mwantum Dau.

Kwa upande wake, Mbunge Ng’wasi

Wizara nyeti yaambulia asilimia 0.1 ya bajeti

Inatoka Uk. 6

Kamani alishauri pia sheria ifanyiwe marekebisho ili kuondoa kipengele cha dhamana kwa watu wanaotuhumiwa kwa makosa ya ulawiti na ubakaji.

Mbunge huyo kijana ambaye ni mwanasheria kitaaluma, alisema takwimu zinazotolewa kuhusiana na masuala ya ubakaji, ulawiti na mimba za utotoni, zinatisha na inashangaza kuwa serikali haionyeshi umuhimu wa kupambana na mambo hayo kupitia bajeti ya wizara husika.

Akitoa takwimu, Kamani alirejea taarifa zilizotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Daniel Chiongolo, hivi karibuni kuwa takribani wanafunzi 194 walipewa ujauzito katika kipindi cha mwezi mmoja tu mkoani humo.

Kamani alisema pia kutoka wilayani Ileje inaeleza kuwa jumla ya watoto 170 walipata ujauzito katika kipindi cha miezi mitatu.

“Takwimu za serikali zinaonyesha kuwa kwa mwaka 2022 watoto 1,586 walilawitiwa na watoto 6,927 walibakwa. Ingawa takwimu za 2023 hazijitolewa, lakini hali ya mambo inaonyesha kuwa takwimu hizo zinaongezeka,” alisema.

Aidha, alibainisha kuwa ripoti kutoka Hospitali ya Rungwe zinaonyesha kuwa kati ya Oktoba na Desemba, 2023 jumla ya watoto 394 walio na umri wa chini ya miaka 18 walijifungua hospitalini hapo.

“Wazazi katika maeneo haya wamekiri kuwa wanawapatia watoto wao vidonge vya uzazi wa mpango kwa sababu wamefikia hatua hawajui wafanye nini,” alisema.

Mbunge huyo alieleza kuwa na hofu juu ya mustakabali wa taifa katika mazingira ambayo watoto wanaishi hivi sasa na kubainisha kuwa iwapo hali hiyo itaachwa iendele, itafika mahali sifa ya vijana wote wa Watanзания itakuwa “waliwahi kubakwa au kulawitiwa.”

Katika ushauri wake, mbunge huyo



Bunge

kijana mwanasheria alishauri mabadiliko ya sheria ili kuweka mazingira ambayo yatawafanya watu wanaojihusisha na uhalifu huo kuwa na waoga.

Alishauri kuwa dhamana iondolewe kwa watu wote wanaotuhumiwa na makosa na ulawiti na ubakaji na adhabu kwa watakaopatikanana na hatia iongezwe.

“Mimi ni mwanasheria na ninajua wapo watu watakuja na utetezi wa haki, lakini tukumbuke kuwa hii ni vita, tuongeze adhabu. Kwa mfano yupo mtu mkoani Kilimanjaro alishitakiwa kwa ulawiti, akapewa dhamana. Alipokuwa nje akalawiti watu wengine 18,” alisema.

Aidha, mbunge huyo alishauri kuanzishwa kwa kanzi data itakayokuwa na taarifa za watu wote waliokutwa na hatia ya makosa ya ubakaji na ulawiti na kanzidata hiyo iwe wazi kwa watu wote ili kila mtu apate taarifa hizo.

Mbunge Riziki Lulida alishangaa bajeti ya wizara hiyo kuwa kiduchu, na kwamba Bunge limeminya muda wa kujadili masuala yake – kwamba imepangiwa siku moja tu kujadiliwa na hivyo kutowapa muda wa kutosha wabunge kujadili masuala nyeti ambayo yanaliathiri taifa.

“Hii wizara inashughulika na mambo nyeti sana na sisi tuna mambo mazito ya kushauri, lakini hapa - hii bajeti imefanywa ya siku moja tu, kwangu mimi hii ni peanut (kiduchu sana),” alisema mbunge huyo.

Hata hivyo, pamoja na ukali wote waliouonyesha wabunge hao walipitisha bajeti hiyo bila mabadiliko yoyote.

Habari

Wahariri wawili TEF wang'ara kimataifa

Na Mwandishi WETU

WAHARIRI wawili nguli ambao ni wanachama wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) wamechaguliwa kuongoza vyombo vya habari vya kikanda.

Waliochaguliwa kushika nafasi hizo ni Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, ambaye wiki iliyopita alichaguliwa kuwa Rais wa Jumuiya ya Wahariri Afrika Mashariki (EAES).

Wakati Balile akichaguliwa katika mkutano uliofanyika jijini Accra, Ghana, huko Cape Town, Afrika Kusini, Ernest Sungura alichaguliwa kuongoza mtandao wa Mabaraza Huru ya Habari Afrika (Nimca). Sungura, ambaye ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) pia ni mwanachama wa TEF.

Taarifa iliyotolewa na EAES imeeleza kuwa Balile atashikilia nafasi hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi mwaka 2025.

Pia taarifa hiyo ilieleza kuwa Fitihawok Yewondwoss kutoka Jukwaa la Wahariri la Ethiopia, alichaguliwa kuwa makamu wa rais wa taasisi hiyo ya kikanda katika kipindi kama hicho.

Uchaguzi huo ulifanyika pembeni ya Kongamano la Tatu la Wanahabari Afrika. Kwa mara ya kwanza kongamano hilo lilifanyika mwaka juzi jijini Arusha, Tanzania ambapo Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa mgeni rasmi.

Akizungumza baada ya kupewa wadhifa huo, Balile alisisitiza umuhimu wa uhuru wa kupata habari ikiwa ni haki



Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile.

ya msingi ambayo inawezesha upatikanaji wa haki nyingine za binadamu.

Alisema chini ya uongozi wake, atahakikisha kuwa EAES inafanya kila linalowezekana ili waandishi wa habari na jamii katika eneo la Afrika Mashariki na nje ya hapo, zifaidi matunda ya kuwepo kwa uhuru wa vyombo vya habari.

Alisisitiza umuhimu wa ushirikiano baina ya vyombo vya habari na serikali, vyama vya siasa, vyama vya kijamii na jumuiya ya kimataifa ili kuviwezesha vyombo vya habari kuwa na uendelevu katika utekelezaji wa majukumu yake.

Wakati huohuo, Sungura anakuwa kiongozi wa kwanza wa Nimca ambayo imeundwa mwaka huu baada ya mabaraza hayo ya habari kuona umuhimu wa kuwa na chombo ambacho kitawaunganisha.

Taarifa iliyotolewa baada ya mkutano huo inaeleza kuwa chombo hicho kinaundwa na mabaraza ya habari kutoka nchi 13 za mashariki, magharibi na kusini mwa Afrika.

Nimca iliyaalika mabaraza mengine ya habari kutoka katika nchi nyingine za Afrika kujiunga na umoja huo ili kuongeza nguvu za ushirikiano katika kudai uhuru wa vyombo vya habari Afrika na kuwa na uwezo wa kujidhibiti vyenyele katika utendaji wake.

Nimca inalenga kuona vyombo vya habari Afrika vikifanya kazi zake kwa uhuru bila ya woga.

“Maadili ya Nimca yataongozwa na kauli ya uhuru wa habari duniani na upatikanaji wa habari iliyotolewa na Kamisheni ya Afrika ya Haki za Watu na Binadamu.



Ernest Sungura



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Wanasiasa sasa ongeeni lugha moja

Na Rashid MTAGALUKA

TAKRIBAN miaka 47 ya uhai wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kimefanikiwa kujipambanua kwa umahiri wa kutetea, kupigania na kulinda maslahi ya Watanzania.

Kabla na hata baada ya kuwepo kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa, CCM na viongozi wake wameendelea kuimarisha umoja, upendo na mshikamano wao kitaifa kwa kufanikiwa kuruka viunzi vingi!

Hata hivyo, bado chama hicho kikongwe Afrika kinakabiliwa na changamoto ileile inayoikabili vyama vyote vya siasa hapa nchini ambayo nimewahi kukitahadharisha kupitia safu hii.

Nilisema na naendelea kusema hata leo kwamba CCM pamoja na ukongwe wake na uzoefu mkubwa wa kuongoza serikali tangu ilipoasisiwa, kisipoyapatanisha makundi matatu yaliyomo ndani yake, kisilaumu mtu.

Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kusema kwamba, bila CCM imara nchi itayumba, na hili ndilo linanifanya kila mara kutoa tahadhari kwa viongozi wa chama hicho ambao baadhi yao wameanza kutengezeana 'ajali' za kisiasa ili tusifike huko.

Kuyumba kwa nchi siyo lazima tukuone kukitokea kama vile tunavyokiona kimbunga au tetemeko la ardhi hapana, bali mabadiliko ya mara kwa mara ya uongozi anayofanya Rais Samia Suluhu Hassan ni ishara kwamba, viongozi wengi wanashindwa kufikia matarajio yake, hivyo anajaribu kuwapangua kila mara kutafuta unafuu.

Fikiria wakati Rais Samia anawateua kumsaidia kuwatumikia Watanzania, wao wanatumia fursa hiyo kupanga safu ili warudi tena kwenye walivyonyavyo sasa katika uchaguzi mkuu ujao na baadhi yao wanakwenda mbali zaidi wakiwaza urais



Balosi Dkt. Emmanuel Nchimbi

wa mwaka 2030.

Mbali na hao, wapo wasioangaliana vizuri kama tulivyowahi kusikia kiongozi mmoja wa chama akidai wanaoangusha serikali ya Rais Samia, siyo vyama vya upinzani, bali ni watendaji wabovu wa serikali.

Aidha, kiongozi huyohuyo alipoondolewa ndani ya chama na kupelekwa serikalini akasikika tena hadharani akitoa tuhuma nzito dhidi ya baadhi ya mawaziri kugharamia watu wanaomtukana Rais Samia mitandaoni.

Mara baada ya katibu mkuu mpya wa CCM, Balosi Dkt. Emmanuel Nchimbi kuingia ofisini na kuanza kazi, tukasikia akikemea viongozi wanaomiliki vikosi vya upelelezi dhidi ya wenzao!

Hatujakaa sana, mara tukamsikia Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdurhaman Kinana naye akisema haipendezi kwa viongozi wa chama chake kuwadharahu watendaji wa serikali kwani wao ndio watekelezaji wakubwa wa ilani yao.

Sasa kwa kuwa kila kiongozi anayepata uteuzi anao mtindo wake wa kuongoza, ni vyema viongozi wa CCM ngazi ya taifa wakakubaliana kuwa wamoja zaidi ili kuisaidia nchi kwa kufanya kazi kubwa ya kutumikia umma na kuepuka makundi yanayoweza kugawa nchi.

Rashid Mtagaluka ni Mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu 0784 13 85 46/ mtagaluka@gmail.com

Kenya

Bunge Marekani lagoma kumwalika Ruto

Na Julius MKAMBI,
Nairobi

OMBI la kumwalika Rais wa Kenya, William Ruto kuhutubia Bunge la Marekani, limegonga mwamba.

Spika wa Bunge la Marekani, Mike Johnson, amekataa ombi la Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya Kigeni, Michael McCaul, na mjumbe wa kamati hiyo, Gregory Meeks, kumwalika Rais Ruto kuhutubia.

Rais Ruto alitarajiwa kulihutubia bunge hilo laiti ombi lingekubaliwa wakati atakapofanya ziara nchini Marekani Alahamisi ya wiki hii -Mei 23 mwaka huu kufuatia mwaliko maalumu wa Rais wa Marekani, Joe Biden.

“Tunaandika kukuomba kwa heshima utoe mwaliko rasmi kwa Rais wa Jamhuri ya Kenya, William Samoei Ruto, kuhutubia kikao cha pamoja cha Congress katika ziara yake rasmi Marekani,” ilisomeka sehemu ya barua iliyoandikwa na wabunge hao kwenda kwa Spika.

Kwa kawaida kikao cha pamoja cha Congress hufanyika wakati mtu mashuhuri, mara nyingi kiongozi wa nchi ya kigeni, anapoalikwa kuhutubia Bunge na Seneti kwa wakati mmoja.

Ifahamike ili rais wa taifa la kigeni aweze kuhutubia mkutano wa pamoja wa Congress, lazima kuwe na maafikiano ya jumla kati ya Bunge na Seneti yatakayolenga kupatikana kwa mwaliko wa pekee.

Hivyo basi, kitendo cha Spika wa Marekani Johnson kukataa ombi la kuruhusiwa kwa Rais Ruto kuhutubia Bunge, kumemkoshesha fursa ya kuwa kiongozi wa kwanza kutoka Kenya, na wa tatu kutoka Afrika kufanya hivyo.

Viongozi wa Afrika waliyowahi kuhutubia Bunge la Marekani ni aliyekuwa Rais wa Liberia, Ellen Sirleaf Johnson mwaka 2006 na Rais wa zamani



Rais wa Kenya, William Ruto

wa Afrika Kusini Nelson Mandela katika miaka ya 1990.

Rais Biden na mkewe Jill Biden watakuwa wenyeji wa Rais Ruto na mkewe Rachel Ruto kwenye ziara ambayo inaendana na maadhimisho ya miaka 60 ya uhusiano wa kidiplomasia kati ya Marekani na Kenya.

“Ziara hiyo itaimarisha dhamira yetu ya pamoja ya kuendeleza amani na usalama, kupanua uhusiano wetu wa kiuchumi, na kusimama pamoja katika kulinda maadili ya kidemokrasia,” ilisomeka sehemu ya taarifa kutoka Ikulu ya Marekani kuhusiana na ziara hiyo ya Rais Ruto.

Pamoja na mambo mengine, viongozi hao watajadili njia za kuimarisha ushirikiano katika maeneo kadhaa ikiwa ni pamoja na uhusiano kati ya watu wa nchi hizo, biashara na uwekezaji, uvumbuzi wa kiteknolojia, hali ya hewa na nishati safi, afya na usalama.

Rais Ruto anatazamiwa kwenye ziara yake hiyo kujadili kurefushwa kwa mkataba wa kibiasara kati ya Marekani na Afrika ikizingatiwa nchi za Afrika zinanufaika zaidi na Sheria ya Ukuaji na Fursa ya Afrika (Agoa) inayotarajiwa kumalizika mwakani.

BoT yawafundisha viziwi kutambua noti

Na Mwandishi WETU,
Geita

WATU wenye ulemavu wa kusikia katika Mkoa wa Geita, wameapatiwa mafunzo maalum ya kuwawezesha kuzitambua fedha zenye mfumo wa noti, na thamani yake.

Mafunzo hayo yalitolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa ushirikiano na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita na Taasisi ya Maendeleo ya Viziwi Tanzania (Tamivita).

Akifungua mafunzo hayo kwa niaba ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dkt. Doto Biteko, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis, alisema serikali imeendelea kuweka kipaumbele masuala ya watu wenye ulemavu katika masuala ya elimu, uwezesaji kiuchumi, afya, ajira, nyenzo za kujimudu pamoja na mafunzo ya ufundi stadi, kwa lengo la kuwawezesha na kuwaunganisha na fursa zilizopo katika jamii.

“Serikali inatambua kuwa watu wenye ulemavu, wakiwemo viziwi, bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazosababisha wengi wao kutofikia malengo yao,” aliongeza.

Alisema serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali sambamba na kutekeleza matakwa ya Sheria ya Watu wenye Ulemavu Namba 9 ya mwaka 2010 na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu kupitia utekelezaji wa Iiani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya 2020 – 2025.

“Nitumie fursa hii kuwashukuru wadau wa maendeleo mlioshiriki kuandaa mafunzo ya kuwajengea uwezo watu wenye ulemavu na ni dhahiri mmekuwa mstari wa mbele kuunga mkono jitihada za Dkt. Samia Suluhu Hassan, zinazolenga kumuwezesha kila



Noti

mwananchi na hali yake kupata huduma stahiki na kwa wakati,” alisisitiza.

Aidha, alilitaka kundi hilo kuchangamkia fursa za fedha zinazotolewa kupitia wizara hiyo ambayo inatoa mikopo yenye masharti nafuu kupitia Benki ya NMB kwa wafanyabiashara wadogo na kuweka bayana kwamba kiasi cha shilingi bilioni 18.5 zimetengwa na serikali kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wafanyabiashara wadogo.

“Fikeni halmashauri, hususan Ofisi za Maendeleo ya Jamii ili waweze kuwapa utaratibu wa kupata mikopo hiyo. Pia, ninawasihaji mjasijili na kupata vitambulisho vya wajasiriamali wadogo mara vitakapoanza kutolewa ili muweze kukopesheka katika taasisi za fedha na mamlaka za serikali za mitaa,” alisema.

Kwa upande wake, Katibu wa Tamivita Wilaya ya Bukombe, Mkoani Geita, Kevin Nyema, aliishukuru serikali kwa kuwezesha mafunzo hayo yatakayowasaidia viziwi kutambua noti wakati wa shughuli zao mbalimbali za kiuchumi na kuwapa fursa zaidi ya kushiriki katika shughuli hizo kikamilifu.

Mafunzo ya utambuzi wa noti kwa watu wenye ulemavu hususan viziwi, yanaratibiwa na BoT kwa kuzingatia miongozo na kanuni mbalimbali za fedha nchini kwa lengo la kuwapa uwezo kukabili changamoto za kifedha ikiwemo utapeli.

Habari

Majaliwa akemea serikali kuficha taarifa

Na Mwandishi WETU

VIONGOZI na watendaji wa serikali wanaoficha ama kuchelewa kutoa taarifa kwa vyombo vya habari, “wamemchafua” Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Hivyo, amewataka kuacha tabia ya “kuatamia” habari wakati zinatakiwa kuwafikia wananchi.

“Viongozi na watendaji wa serikali na mashirika zingatieni Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa ya Mwaka 2016 na ondoeni ukiritimba katika suala la upatikanaji wa habari ili wanahabari wawezeshwe kupata taarifa sahihi na wafanye kazi zao kwa ufanisi wa hali ya juu,” amesema.

Waziri mkuu alitoa mwito huo Ijumaa iliyopita - Mei 3, 2024 wakati akizungumza na waaandishi wa habari na wadau wengine kwenye maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani yaliyofanyika Mjini Dodoma.

Kuhusu kupata habari sahihi, Majaliwa pia aliwataka wakuu wa taasisi waweke mazingira mazuri kwa waandishi wa habari ili kuwawezesha kuzingatia weledi na kurahisisha kupata taarifa muhimu.

Aidha, alivitaka vyombo vya habari viunde madawati maalum yatakayoratibu masuala ya mabadiliko ya tabianchi.

“Madawati hayo yatafute fedha kwa ajili ya kutekeleza mpango wa mafunzo ya waandishi wa habari kuhusu kuandika kitaalamu masuala ya mabadiliko ya tabianchi na madhara yake kwa jamii na taifa. Suala hili likamilike ili katika maadhimisho ya siku hii mwakani, iwepo taarifa ya utekelezaji,” alisisitiza.

Kuhusu habari za uchunguzi, waziri mkuu amesema uandishi wa habari hizo unahitaji rasilimali fedha za kutosha ili kutoa mafunzo na kuifanya kazi yenyewe.

“Niwaombe wadau wote muhimu wakiwemo taasisi, asasi za kiraia na mashirika mbalimbali ya ndani na nje ya nchi washirikiane na vyombo vya habari



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa

katika kufanikisha utafiti na uandishi wa habari za uchunguzi na kuvisaidea vyombo vya habari kukua kitaaluma na kiuchumi.”

Alitumia fursa hiyo kuwahimiza wanahabari wote wazingatie uzalendo, weledi na maadili ya taaluma ya uandishi kwa kutoa mchango chanya kwa jamii kwani wasipofanya hivyo, tasnia hiyo inaweza kuwa chanzo cha kufifisha maendeleo na hata kuhatarisha amani, umoja na mshikamano wa kitaifa.

Waziri Mkuu Majaliwa alisema vyombo vya habari vinayo nafasi kubwa ya kuitangaza nchi pamoja na kujengea taswira chanya kimataifa na kuwapomgeza wanahabari kwa kazi wanayoifanya ya kuuhabarisha umma.

“Vyombo vya habari vimekuwa na mchango mkubwa katika kuhamasisha uwekezaji, kutangaza vivutio vya utalii na kuchangia katika kuinua uchumi wa taifa letu. Kwa niaba ya serikali na wananchi wote wa Tanzania ninavipongeza sana vyombo vyetu ya habari kwa kazi kubwa inayofanywa katika kuutumikia umma.”

Kaulimbiu ya maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani kwa mwaka 2024 inasema: “Uandishi wa habari na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.”

Muungano wa Tanzania fupa gumu

Na Waandishi WETU

SASA ni dhahiri shahiri kwamba kuna dalili za kutikishwa kwa usalama wa Tanzania.

Dalili hizo zinabebwa na na minyukano ya wazi, na huenda mingi ipo ya kificho, inayotikisa ustawi wa muungano wa nchi mbili; Tanganyika na Zanzibar uliozaa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Chokochocho za kuutikisa Muungano zimeibuka zaidi hivi karibuni, zikipazwa na watu “wakubwa” na mashuhuri wa Tanzania, na hasa wanasiasa, wakiwamo baadhi ya wabunge.

Hawa ni wale walioko ndani ya vyama vya upinzani wanaozungumza waziwazi kwenye mikutano ya hadhara, ndani ya bunge na zaidi kwenye makusanyiko ya watu, maeneo kadhaa, ikiwamo kwenye makongamano.

Pia wamo viongozi wa dini; Wakristo na Waislam ambao nao wamekuwa na mtazamo tofauti kuhusu kuwepo kwa Muungano.

Pambazuko pia limewafikia wanasiasa ndani ya chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambao wao wanazungumza kwa kificho, huku wakiogopa kutajwa majina yao, kwa kuwa wataonekana wasaliti kwa kupingana na msimamo wa chama chao, kinachodai kuwa masuala ya Muungano sasa “yako shwari.”

Waliozungumza na Pambazuko kwa nyakati na maeneo tofauti, wametamani kuitishwa kwa kura ya maoni ili Watanzania waamue hatma ya Muungano ambao sasa umedumu kwa miaka 60 tangu kuasisiwa kwake.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) anasema Muungano umekuwa na mambo mengi ambayo yanakataliwa kwa pamoja na moja kwa moja na wananchi wa Tanganyika na Zanzibar.

Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na muundo wa Muungano wenyewe, ambapo wapo wanaokubaliana kuwepo



Saini

kwa serikali tatu, wengine mbili na baadhi wakitaka kuendelea kuwepo kwa serikali moja.

“Muundo wa Muungano ndiyo unaozungumzwa zaidi, huku wengi kutoka Zanzibar wakitaka kuwepo kwa serikali tatu, yaani Zanzibar iwe na serikali yake, Tanganyika na sasa kuwepo na serikali kuu,” anaongeza Lissu.

Lissu anairejea dhamana iliyobebwa na Tume Mabadiliko ya Katiba chini ya Jaji Joseph Warioba ambayo ilikuja na matamano makubwa ya Watanzania aliohojiwa juu ya muundo wa Muungano wa kuwa na serikali tatu.

Kiongozi huyo wa Chadema anadai Muungano ni kiini macho kwa kuwa ni kama ulifanyika kwa kulazimisha maana sasa wananchi wengi wa kila upande wanalalamika.

Katibu Mkuu wa Shura ya Maimama Tanzania, Sheikh Ponda Issa Ponda anasema Muungano unaonekana “kukosa baraka za watu wengi kutoka kila upande,” huku akidai kuwa umebeba mambo kadhaa yaliyofichwa.

Sheikh Ponda anasema Muungano ulivyo hivi sasa - wa serikali moja, hauna afya, hivyo kuhitaji maboresho makubwa ili unufaishe kila upande na kuondoa manung'uniko.

Anatoa mwito kwa serikali kuangalia namna ya kuitisha kura ya maoni haraka ili kila upande ujue wananchi wake

Inaendelea Uk. 14

Habari

Muungano wa Tanzania fupa gumu

Inatoka Uk. 13

wanapenda muungano wa namna gani.

Mhadhiri wa vyuo vikuu kadhaa, Dkt. Lenny Kasoga anaeleza kuwa chokochocho kuhusu Muungano zimeivuka kwa nguvu na kuhoji “kwanini sasa?”

Msomi huyo wa siasa na uchumi anasema kuwepo kwa chokochocho hizo kwanza kunatishia usalama wa taifa na kuwa ni mthani mkubwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye amerithi “mikoba ya urais” baada ya kifo cha John Magufuli aliyekuwa rais hadi Machi 18, 2021.

Anasema hivi karibuni ameshangazwa na kuwepo mazingira ya kuuchoka Muungano, siyo kutoka kwa Wazanzibari pekee, bali hata Watanganyika.

“Nimesikia mara nyingi, tena hivi karibuni mambo mengi yanayoashiria kuchokwa kwa Muungano yakiibuka, hii maana yake ni kuwa wananchi wanataka mabadiliko na ni vyema wakasikilizwa,” ameongeza Dkt. Kasoga ambaye amewahi kufundisha vyuo kadhaa Marekani kabla ya kurejea Tanzania na kufundisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Hivi karibuni, wabunge kadhaa kutoka Zanzibar walilalamika kuwepo kwa vitendo vinavyoashiria kubaguliwa kwa Wazanzibari ndani ya Tanzania na mwingine akishauri kuwepo kwa utaratibu wa kutumia pasi za kusafiria kwa Watanganyika (Watanzania Bara) wanaposafiri kuingia Zanzibar.

Tangu kuasisiwa kwa Muungano huo, kumekuwapo kwa changamoto nyingi za kiutendaji na kimamlaka, ambapo zilibatizwa jina la “Kero za Muungano,” na kwamba zimekuwa zikipatiwa ufumbuzi siku hadi siku kwa miaka yote hiyo 60 ya uhai wake.

Wachambuzi wengi wa siasa wanalaumu Zanzibar kuwa chanzo cha kuitikisa Muungano kwani imebadili katiba yake, bila kuweka mambo kadhaa yaliyokubaliwa kwenye Hati za Muungano.

Kwamba ndani ya Katiba ya Zanzibar iliyobadilishwa mwaka 1984, inaipa hadhi kuwa nchi, wakati awali ilitanabaishwa



Kuchanganya udongo

kuwa sehemu ya Tanzania.

Jaji Warioba hivi karibuni akiwa Dodoma alisema mambo kadhaa yaliyokuwa kwenye makubaliano ya kuwa ya Tanzania, sasa Zanzibar imeyaacha na “inafanya mambo yake mengi ya Muungano yenyewe.”

Kuundwa kwa Muungano

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliundwa Aprili 26, 1964 ikiwa ni muungano wa mataifa mawili huru ya Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ambayo yaliingia mkataba wa kuungana mwaka 1964 na kuanzishwa Dola ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mkataba wa Muungano ulitiwa saini na aliyekuwa Rais wa Tanganyika, Mwalimu Julius Nyerere na aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume, Aprili 22, 1964 huko Zanzibar.

Mkataba huo ulithibitishwa na Bunge la Tanganyika na Baraza la Mapinduzi hapo Aprili 26, 1964. Tarehe 27 Aprili, 1964, viongozi wa nchi zote mbili walikutana katika ukumbi wa Karimjee Jijini Dar es Salaam na kubadilishana Hati za Muungano.

Jina hili la “Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar” lilibadilishwa baadaye Oktoba 28, 1964 na kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia Sheria ya Jamhuri ya Muungano, Sheria namba 61 ya mwaka 1964.

Sababu za kuwepo kwa Muungano

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umekuwapo kutokana na sababu



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au
Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Habari**Muungano wa Tanzania fupa gumu***Inatoka Uk. 14*

mbalimbali kama vile kuwepo kwa uhusiano wa karibu na ya kihistoria baina ya Tanganyika na Zanzibar katika nyanja mbalimbali kama vile udugu wa damu, biashara, utamaduni, lugha na uhusiano wa karibu kisiasa hususan baina ya vyama vya TANU na ASP

Pia, azma ya kuwa na Muungano wa Afrika hususan kwa kuanzia na Shirikisho la Afrika Mashariki. Hata kabla ya uhuru wa Tanganyika, Mwalimu Nyerere pamoja na viongozi wengine waliokuwa wakipigania uhuru katika ukanda wa Afrika walikuwa na matarajio ya kuwa na Muungano wa Afrika. Mwalimu Nyerere binafsi alipendelea uwepo Muungano wa Afrika kwa kuanzia na Mashirikisho ya kikanda.

Kimsingi, zipo sababu mbalimbali zilizosababisha Muungano huu kama vile historia za nchi hizi mbili, ukaribu wa nchi hizi mbili, muingiliano wa kijamii, ushirikiano wa kibashara, ushirikiano madhubuti na wa muda mrefu wa kisiasa baina ya TANU na ASP ushirikiano na urafiki wa muda mrefu kati ya watu, viongozi, na wakati wa harakati za utafu uliopelekea uhuru wa nchi hizo mbili.

Hati ya Makubaliano ya Muungano

Msingi wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ni Hati za Muungano za mwaka 1964. Hati za Muungano zilitiwa saini na waasisi wa Muungano Aprili 22, 1964, na kusababisha Tanganyika na Zanzibar kuwa dola moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Baada ya Muungano, Mwalimu Nyerere alikuwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheikh Abeid Amani Karume, alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aprili 26, 1964 Bunge la Tanganyika lilipitisha Sheria za Muungano. Halikadhalika, Sheria hizi zilithibitishwa na Baraza la Mapinduzi Zanzibar.

Sheria hizi za Muungano zilithibitisha Hati za Muungano, zilitaja Rais na

*Bendera ya Tanzania*

Makamu wa Rais, zilitaja Muundo wa Muungano na Katiba ya Muungano.

Aidha, Aprili 27, 1964, waasisi wa Muungano walibadilishana Hati za Muungano na wajumbe saba wa Baraza la Mapinduzi waliapishwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao ni Sheikh Abeid Amani Karume, Kassim Abdala Hanga, Abdulrahman Mohamed Babu, Hassan Nassor Moyo, Sheikh Aboud Jumbe, Hasnu Makame na Sheikh Idris Abdul Wakil. Baada ya kuapishwa kuwa Wabunge wakateuliwa kuwa Mawaziri wa Serikali ya Muungano.

Kabla ya Muungano, kulikuwa na Katiba ya Tanganyika ya mwaka 1962 na upande wa Zanzibar kulikuwa na Amri za Katiba (Decrees).

Katiba ya Tanganyika baada ya kufanyiwa marekebisho ili kukidhi mahitaji ya Muungano, iliendelea kutumika kama Katiba ya Muungano ya mpito hadi mwaka 1977 ilipopitishwa Katiba ya Muungano kwa mujibu wa Makubaliano ya Muungano na Sheria za Muungano.

Aidha, marekebisho hayo yalimtaja Rais wa Zanzibar kuwa ni Makamu wa Kwanza wa Rais, akiwa ni msaidizi wa Rais kwa masuala yote ya kiutawala kwa upande wa Zanzibar, na Waziri Mkuu kuwa ni Makamu wa Pili wa Rais ambaye atamsaidia Rais kwa masuala yahasuyo upande wa Tanganyika na kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni.

Katiba ya muda ya mwaka 1965 ya

Muungano wa Tanzania fupa gumu

Inatoka Uk. 16

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliainisha mambo kumi na moja ambayo yalikulibika kuwa ni ya Muungano chini ya usimamizi wa Serikali ya Muungano ambayo ni pamoja na Katiba na Serikali ya Muungano Mambo hayo ni: - Mambo ya Nchi za Nje; Ulinzi; Polisi; Mamlaka juu ya mambo yanohusika na hali ya hatari; Uraia; Uhamiaji; Mikopo na Biashara ya Nchi za Nje na Utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano.


Mambo mengine ni Kodi ya Mapato inayolipwa na watu binafsi na mashirika, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania unaosimamiwa na Idara ya Forodha; na Bandari, mambo yanayohusika na usafiri wa anga, posta na simu.

Kuongezeka kwa Orodha ya Mambo ya Muungano

Mambo ya Muungano yaliongezwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria na kwa kushirikisha pande zote mbili za Muungano. Juni 10, 1965, mambo yote yahasuyo sarafu na fedha kwa ajili ya malipo yoyote halali (pamoja na noti); mabanki (pamoja na mabanki ya kuweka akiba) na shughuli zote za mabanki; fedha za kigeni na usimamizi juu ya mambo yanayohusu fedha za kigeni yaliingizwa kuwa jambo la 12 la Muungano.

Lengo kubwa la kuongezwa kwa jambo hilo ilikuwa ni kuwa na sarafu ya pamoja ya Tanzania baada ya Muungano, na kurahisisha usimamizi wa fedha za kigeni na mabanki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufuatia kuvunjika kwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki mwaka 1964.

Baada ya kuvunjika kwa Bodi hiyo, kila nchi mwanachama wa Jumuiya ililazimika kuwa na sarafu na mipango yake ya kusimamia mambo ya kibenki na fedha. Kufuatia kuundwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1967, tarehe 11 Agosti, 1967 mambo mawili yaliongezwa katika orodha ya Mambo ya Muungano ambayo ni leseni za viwanda na takwimu (Jambo la 13), na elimu ya juu (Jambo



Saini za waasisi wa muungano

la 14).

Mwaka 1968, suala la maliasili ya mafuta pamoja na mafuta yasiyochujwa ya motokaa na mafuta ya aina ya petroli na aina nyinginezo za mafuta au bidhaa na gesi asilia liliongezwa kwenye Orodha ya Mambo ya Muungano kuwa Jambo la 15. Vilevile, kufuatia kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977 na kutungwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, mambo yafuatayo yaliongezwa katika Orodha ya Mambo ya Muungano ambayo ni Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania na mambo yanayohusika na kazi za Baraza hilo (Jambo la 16); Usafiri; Usafirishaji wa Anga (Jambo la 17) na Utafiti (Jambo la 18); Utabiri wa Hali ya Hewa (Jambo la 19); na Takwimu (Jambo la 20). Kutokana na kuvunjika kwa Mahakama ya Rufani ya Afrika Mashariki mwaka 1979, suala la Mahakama ya Rufani ya Tanzania nalo liliongezwa katika Orodha ya Mambo ya Muungano na kuwa Jambo la 21. Vilevile, kufuatia mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Nyalali iliyokusanya maoni ya kuanzishwa kwa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa, Uandikishaji wa Vyama vya Siasa na mambo mengine yanayohusiana nayo liliongezwa kwenye Orodha ya Mambo ya Muungano (Jambo la 22). Suala hilo hatimaye lilipitishwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura Namba 258. Utaratibu uliotumika katika kuongeza idadi ya mambo ya Muungano kutoka 11 hadi kufikia 22 ni kupitia maamuzi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Congo

Rais Tshisekedi chupuchupu kupinduliwa

Na Mwandishi WETU

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi amenusurika kuondolewa madarakani katika mapinduzi ya kijeshi ambayo yamezimwa na sehemu nyingine ya jeshi la nchi hiyo.

Taarifa ya jana kutoka jijini Kinshasa, zinaeleza kuwa watu kadhaa waliuawa katika harakati za mapinduzi hayo kutokana na mapigano yaliyotokea baina ya kundi moja la wanajeshi na linguine ambalo halikuwa na utawali wa kuasi.

Aidha, watu kadhaa, wakiwamo raia wa kigeni, inaelezwa kuwa wamekamatwa kwa tuhuma za kupanga na kutekelea mapinduzi hayo.

Taarifa iliyotolewa na jeshi inaeleza kuwa mapinduzi hayo yalipangwa na watu raia wa DRC wakishirikiana na baadhi ya raia wa kigeni ambao alfajiri ya Jumapili walivamia makazi ya mmoja wa washirika wa karibu wa Rais Tshisekedi, Vital Kamerhe, jijini Kinshasa.

Baada ya risasi kufyatuliwa katika maeneo kadhaa kuzunguka makazi ya kiongozi huyo kutoka chama tawala, hatimaye jeshi likatangaza Jumapili asubuhi kuwa limefanikiwa kuzima mapinduzi hayo na kuwakamata watu kadhaa.

Kwa mujibu wa shirika la habari la AP, watu watatu walifariki kufuatia ufyatulianaji wa risasi kati ya watu wenye silaha waliovalia sare za kijeshi na watu wanaoaminiwa kuwa walinzi wa mwanasiasa Kamerhe katika mji mkuu, Kinshasa.

“Jaribio la mapinduzi ya kijeshi lililochochewa limetibuliwa na vikosi vya alinzi na usalama vya Congo na hali sasa imedhibitiwa,” msemaji wa jeshi la Congo, Brigedia Jenerali Sylvain Ekenge, aliwaambia waandishi wa habari jana asubuhi.



Raia Felix Tshisekedi

Habari kuhusu mapinduzi hayo zinakuja wakati ambapo chama tawala cha Rais Tshisekedi kikiwa kwenye mgogoro mzito wa kiongozi baada ya vigogo katika chama hicho kutokubaliana na utaratibu wa uchaguzi wa viongozi wa Bunge la Taifa na nafasi nyingine nyeti serikalini.

Uchaguzi wa Spika wa Bunge ulipangwa kufanyika Jumamosi iliyopita, lakini ukaaahirishwa kutokana na migongano ndani ya chama tawala ambacho kilishinda uchaguzi mkuu uliofanyika Desemba mwaka jana.

Kamerhe ni mmoja wa wanasiasa wenye nguvu nchini DRC na anatajwa kama mtu mwenye nafasi kubwa ya kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Shirikisho.

Taarifa iliyotolewa na msemaji wa mwanasiasa huyo, Michel Moto Muhima, kupitia mtandao wa X, inasema kuwa Kamerhe na familia yake wapo salama.

Kati ya watu watatu waliouawa mmoja anatajwa kuwa ni kati ya wavamizi hao na wawili ni askari kutoka jeshi la polisi nchini humo.

Tshisekedi alishinda urais kwa mara ya pili mfululizo katika uchaguzi uliofanyika Desemba mwaka jana. Uchaguzi huo ulikabiliwa na vurugu katika baadhi ya sehemu ingawa kwa ujumla ilielezwa kuwa ulikuwa wa utulivu.

TFF lawamani msiba wa Jellah Mtagwa

Na Rashid MTAGALUKA,
Morogoro.

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limeingia lawamani kwa “kutelekeza” msiba wa mwanakabumbu mahiri, Jellah Abdallah Mtagwa.

Baadhi ya wachezaji wa zamani wa Taifa Stars waliowahi kucheza pamoja na Mtagwa wameeleza kusikitishwa baada ya TFF kuwa na ushiriki hafifu na kushindwa kulinda hadhi ya Mtagwa hata wakati wa maziko yake.

Jellah Mtagwa alizikwa juzi -Jumamosi katika eneo la makaburi ya familia yake Kihonda-Manyuki, Mjini Morogoro.

Wakizunguma na Pambazuko kando ya mazishi hayo, Zamoyoni Mogella, Hussein Ngulungu na Peter Tinho, walisema Mtagwa alikuwa mchezaji aliyeiletea heshima Tanzania wakati wa mashindano ya makubwa ya kwanza ya Afrika mwaka 1980.

Kwamba kwa ukuu wake na sifa alizotea Tanzania, alipaswa kuzikwa kwa heshima kubwa, zilizosimamiwa na serikali kupitia TFF.

“Mwaka 1980 Jellah akiwa nahodha, alikiongoza kikosi cha timu ya taifa katika fainali ya mashindano ya Kombe la Afcon yaliyofanyika kwa mara ya kwanza nchini Nigeria, lakini leo anazikwa kwa hadhi hafifu”, alisema Mogella.

Mogella alisema inasikitisha kuona nchi haithamini vipaji vya wachezaji wake wanapokuwa wanaumwa na kibaya zaidi, inawatelekeza wanapofariki dunia.

Anakumbuka ukuu wa Mtagwa kwa kueleza kuwa mwaka 1974 picha yake iliwekwa kwenye stamp na kuwa rafiki yake huyo alizunguka karibu dunia nzima akiitangaza Tanzania.

“Hapa naona kuna unyonge fulani hivi katika msiba wa Jellah, nchi haithamini, hakika TFF na serikali wanavunja moyo wanamichezo, hasa kizazi hiki kinachokuja kuturithi, sisi, kikiona haya,



Jellah Abdallah Mtagwa

kinakata tama kabisa,” alisema Mongella.

Naye Peter Tinho alisema Mtagwa, licha kuwahi kucheza timu za ndani ya Tanzania, lakini amekuwa miongoni mwa wachezaji wasiofutika katika historia ya soka, hivyo angepaswa kupewa heshima kubwa wakati wa ugonjwa na hata anapozikwa.

“Jellah amefanya makubwa sana katika nchi yetu hii, hasa kwenye soka, alikuwa nahodha katika timu ya Taifa, unajua miaka ile ya 1974 mtu kuchapishwa picha yake kwenye stamp siyo mchezo”, alisisitiza Tinho kwa masikitiko.

Tinho alisema mazishi ya Mtagwa yalitakiwa ‘kubebwa’ na serikali kupitia TFF kutokana na mchango wake mkubwa na heshima ambayo aliiletea Tanzania kupitia mchezo wa mpira wa miguu.

Aliyewahi kuwa Rais wa TFF ambaye pia alicheza pamoja na Mtagwa katika timu ya taifa, Leonard Ledger Tenga, aliliambia Pambazuko kuwa, Tanzania imepoteza mtu muhimu aliyecheza na zaidi kupenda soka.

Mtwaga aliwahi kuchezea Nyota, Tumbaku zote za mjini Morogoro na Pan Africa na Yanga za Dar es Salaam.

Alifariki Mei 16, 2024 katika Hospitali ya Mloganzila, Dar es Salaam na kuzikwa siku iliyofuata. Ameacha mke, watoto wanne wa wajukuu kadhaa.

Lissu akiangalia matundu ya risasi...



Makamu Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu Ijumaa ilyopita alikabidhiwa gari lake aina ya Toyota Land Cruiser V8 -VXR baada ya kukaa Kituo Kikuu cha Jeshi la Polisi, Dodoma kwa zaidi ya miaka saba. Gari hilo limekuwepo hapo tangu Septemba 7, 2017, siku aliposhambuliwa kwa risasi. (Picha na Mpigapicha Maalum).

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa msunguko - kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

